SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO ZANZIBAR

BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020

JUNI, 2019

Yaliyomo **Ukurasa**

A. UTANGULIZI 1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA 2
C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2018/2019 4
C.1 Ukusanyaji wa Mapato yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango 4
C.2 Uchambuzi wa Mapato ya ndani 6
C.3 Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango 7
C.4 Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Fedha na Mipango 8
C.4.1 Programu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma 8
C.4.1.1 Pogramu ndogo Usimamizi wa Hazina 8
C.4.1.2 Pogramu ndogo Usimamizi wa Bajeti 10
C.4.1.3 Pogramu ndogo Uratibu wa Fedha za Nje 11
C.4.1.4 Pogramu ndogo ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani 13
C.4.1.5 Pogramu ndogo Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi 13
C.4.2 Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma 15
C.4.2.1 Programu ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma..... 15
C.4.2.2 Programu ndogo ya Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali 16
C.4.3 Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha 17
C.4.3.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara-Unguja 17
C.4.3.2 Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 18

C.4.3.3 Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Wizara-Pemba 19
C.4.4 Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali. 21
C.4.5 Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi 22
C.4.5.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini 22
C.4.5.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu 24
C.4.5.3 Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo 24
C.4.6 Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu 26
C.4.6.1 Programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi 26
C.4.6.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi 27
C.4.6.3 Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali 27
C.4.7 Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango 28
C.4.7.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango 29
C.4.7.2 Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango-Pemba 29

D. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2018 – MACHI 2019 30
D.1 Mradi wa Kuimarisha Huduma Za Jamii Mijini (ZUSP). 30
D.2 Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali 32
D.3 Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Mali Asili (ISP-DRMNRG) 32
D.4 Mradi wa Uimarishaji Utawala Bora Awamu ya tatu (ISPGG III) 33

D.5 Mradi wa Kuendeleza Bandari ya Mangapwani 34
D.6 Mradi wa Kupunguza Umasikini 35
D.7 Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini 35

E. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA 36
E.1 Bodi ya Mapato-Zanzibar (ZRB) 36
E.2 Mfuko wa Barabara (ZRF) 37
E.3 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA) 39
E.4 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma 40
E.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) 41
E.6 Shirika la Bima (ZIC) 43
E.7 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) 44

F. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020 45
F.1 Vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2019/2020 45
F.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019-2020 46
F.2.1 Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma 46
F.2.2 Programu ya Uwekezaji wa Mali za Umma 47
F.2.3 Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango 47
F.2.4 Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali. 48
F.2.5 Programu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi 48
F.2.6 Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu 49
F.2.7 Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango 49

G. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2019/2020 KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA 50
G.1 Bodi ya Mapato-Zanzibar (ZRB) 50
G.2 Mfuko wa Barabara (ZRF) 51
G.3 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA) 52
G.4 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma 53
G.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) 54
G.6 Shirika la Bima (ZIC) 55
G.7 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) 56

H. SHUKRANI 57

I. HITIMISHO 58

J. VIAMBATANISHO VYA UTEKELEZAJI JULAI 2018-MACHI 2019 60
Jadweli nam.1 61
Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango 61
Jadweli nam.2 62
Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2018-Machi 2019 62
J.1 Jadweli nam.3. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya ndani kuelekea 2020 63
Jadweli nam.4 64
Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango Julai 2018-Machi 2019 64
Jadweli nam.5 65
Matumizi ya Wizara kwa Programu-Julai 2018-Machi 2019 65

K. VIAMBATANISHO VINAVYOHUSU MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019-2020 66
VIFUPISHO 70

A. UTANGULIZI

1.0 **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae ili lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

2.0 **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru MwenyeziMungu-Subhana Wataala, kwa kutujaalia sote kuwepo hapa leo hii tukiwa na afya njema, amani na utulivu katika nchi yetu. Hii imetuwezesha kukutana na kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2019-2020.

3.0 **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt.Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara ya Fedha na Mipango. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake uliotukuka wenye dhamira ya dhati ya kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli. Aidha, namshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa uongozi na mashirikiano anayotupatia katika kutekeleza shughuli za Wizara.

4.0 **Mheshimiwa Spika,** katika Baraza lako hili tukufu, nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na wenyeviti wa Baraza, Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar na Mwanasha Khamis Juma,

kwa mnavyoliongoza vyema Baraza hili na jinsi mnavyoshirikiana nasi wakati wote.

5.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya pekee kabisa naomba niishukuru kwa dhati Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Makamu na wajumbe wake wote. Wizara yangu imeendelea kufaidika sana na uongozi wao wenye dira ya kuona mbali, dhamira ya dhati ya kuwatumikia wananchi na kwa ushauri na mashirikiano wanayotupatia katika kutekeleza majukumu na kazi za Wizara. Mimi binafsi na Wizara hii kwa ujumla tunaithamini sana michango yao, maoni na mapendekezo yote na miongozo wanayotupatia katika kutekeleza majukumu yetu.

B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

6.0 **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia Mafungu matatu ya Bajeti ambayo ni: F01-Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu F02- Mfuko Mkuu wa Serikali na F03- Tume ya Mipango. Kimuundo, Wizara inatekeleza majukumu yake kupitia Idara kumi za Wizara, Idara tano za Tume ya Mipango na Taasisi nane zinazojitegemea. Orodha ya Idara na Taasisi hizo ni kama zinavyoonekana katika Jadweli nam.1.

7.0 **Mheshimiwa Spika,** kutokana na ugawaji wa majukumu Serikalini, Wizara inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:

i. Kusimamia mapato ya Serikali kutokana na vyanzo vya ndani na nje ya nchi: Mapato ya

ndani yanahusisha Kodi na mapato yasiyo ya kodi kutokana na vyanzo vya SMZ na vile vya Kodi za Muungano zinazokusanywa Zanzibar. Mapato ya nje ni pamoja na Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Mashirika ya Kimataifa na nchi wahisani;

ii. Kusimamia Mali za Serikali: Jukumu hili linahusisha usimamizi wa masuala ya Ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Serikali pamoja na Mitaji ya Umma kupitia Hisa za SMZ katika Mashirika yake na Kampuni binafsi.

iii. Kusimamia Fedha za Umma na shughuli za Uhasibu Serikalini: chini ya jukumu hili, Wizara ndio msimamizi mkuu wa masuala ya Bajeti ya Serikali, Hazina ya Serikali, Ukaguzi wa Ndani na huduma zote za Uhasibu Serikalini;

iv. Usimamizi wa Deni la Taifa: Wizara inasimamia mwenendo wa Deni la Taifa kutokana na Mikopo ya Ndani na Nje na kutoa ushauri unaopaswa kwa Serikali;

v. kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha: inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na Soko la Hisa na Mitaji pamoja na usimamizi wa Taasisi za huduma ndogo ndogo za Fedha; na

vi. Kushajiisha na kufanikisha uwekezaji binafsi kutoka nje na ndani ya nchi: kwa kutambua umuhimu wa uwekezaji binafsi, Wizara ina jukumu la kushajiisha, kufanikisha na kulinda uwekezaji wa Mitaji binafsi hapa nchini.

8.0 **Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na Mipango Mikuu ya Maendeleo, kupitia Tume ya Mipango, Wizara inatekeleza majukumu yafuatayo:

vii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira Kuu ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye Mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia mahitaji ya makundi tofauti ya watu;

viii. Kuratibu Sera za Kisekta na upunguzaji wa umaskini nchini;

ix. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi; na

x. Kusimamia maendeleo ya Uchumi.

9.0 **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo mafupi ya utangulizi naomba sasa nieleze utekelezaji wa Wizara kwa miezi tisa ya mwanzo ya mwaka wa Fedha unaoendelea (Julai 2018-Machi 2019).

C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2018/2019.

C.1 Ukusanyaji wa Mapato yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

10.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 1,273.74 bilioni ikijumuisha:

i. Mapato ya kodi ya TZS 727.50 bilioni;

ii. TZS 464.20 bilioni ikiwa ni mikopo na ruzuku zinazotarajiwa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

iii. Mapato yasiyo ya kodi ni TZS 42.0 bilioni; na

iv. TZS 40.0 bilioni zilipangwa kukopwa kutoka soko la Fedha la ndani ya nchi.

11.0 Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2018- Machi 2019, Mapato yaliyokusanywa na kuingizwa katika hesabu za Wizara ni TZS 831.92 bilioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya miezi tisa. Mapato haya yametokana na vyanzo vifuatavyo:

i. Mapato yaliyotokana na vyanzo vya kodi ni TZS 511.36 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya miezi tisa ya kukusanya TZS 551.24 bilioni ;

ii. Mikopo kutoka soko la Fedha la ndani ni TZS 32.00 bilioni sawa na asilimia 107 ya makadirio ya kukusanya TZS 30.00 bilioni;

iii. Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 247.97 bilioni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya TZS 348.08 bilioni zilizopangwa kupokelewa kwa kipindi cha miezi tisa; na

iv. Mapato kutokana na vyanzo visivyokua vya kodi ni TZS 41.00 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio ya mwaka ya TZS 38.00 bilioni.

C.2 Uchambuzi wa Mapato ya ndani

12.0 Mheshimiwa Spika, Kati ya mapato ya kodi ya TZS 511.36 bilioni;

Bodi ya Mapato imekusanya TZS 281.09 bilioni sawa asilimia 89 ya makadirio ya kukusanya TZS 314.44 bilioni. Mapato haya yameonesha ukuaji wa asilimia 23 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2017-Machi 2018 ambapo jumla ya TZS 228.03 bilioni zilikusanywa.

13.0 Mheshimiwa Spika, TRA tawi la Zanzibar ilikusanya TZS 216.27 bilioni sawa asilimia 98 ya makadirio ya kukusanya TZS 221.05 bilioni kwa miezi tisa. Mapato haya yanajumuisha TZS 117.50 bilioni zilizokusanywa na Idara ya Forodha na TZS 98.77 bilioni zilikusanywa na Idara ya Kodi za ndani (Domestic Revenue Department). Mapato yaliyokusanywa na taasisi hii yameonesha ukuaji wa asilimia 13.5 ikilinganishwa na mapato ya TZS 190.51 bilioni yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2017 – Machi 2018.

14.0 Mheshimiwa Spika, Mapato kutokana na vyanzo visivyokua vya kodi vinavyosimamiwa na Wizara ni TZS 41.00 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio ya kukusanya TZS 38.0 bilioni kwa miezi tisa ambao uchambuzi wake umeambatanishwa katika Jadweli nam.4. Kwa ujumla ukusanyaji wa Mapato ulikuwa mzuri pamoja na kutofikiwa Malengo.

15.0 Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea TZS 247.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikijumuisha Mikopo ya TZS 218.17 bilioni na Ruzuku za TZS 29.8 bilioni.

Fedha hizi ni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya miezi tisa. Bado chanzo hiki kimeendelea kuathiriwa na kutotekelezwa kwa baadhi ya Miradi mikubwa kama vile:

i. Mradi wa ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal II) uliokadiriwa kupokea TZS 86.3 bilioni kutoka Exim Bank ya China;

ii. Ujenzi wa Hospitali ya Binguni uliokadiriwa kupokea TZS 10.0 bilioni;

iii. Mradi wa kuendeleza na Kuimarisha mazao ya Bahari ulikadiriwa kupokea TZS 6.7 bilioni; na

iv. Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi uliotarajiwa kupokea TZS 6.7 bilioni kutoka kwa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

C.3 Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

16.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilipangiwa kutekeleza Programu kuu saba zikiwa na Programu ndogo kumi na saba pamoja na Miradi kumi na tatu, ambayo ilikadiriwa kutumia TZS 295.61 bilioni. Matumizi halisi kwa kipindi hicho yalifikia TZS 192.26 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya TZS 202.04 bilioni kwa miezi tisa, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Matumizi kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa Wizara ni TZS 6.20 bilioni;

ii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 110.03 bilioni;

iii. Matumizi ya uendeshaji wa kazi za kawaida ni TZS 10.01 bilioni;

iv. Ruzuku zilizotolewa kwa taasisi zilizopo chini ya Wizara ni TZS 27.02 bilioni; na

v. Fedha zilizotumika kutekeleza kazi za miradi ya Maendeleo ni TZS 39.00 bilioni.

C.4 Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Fedha na Mipango.

C.4.1 Programu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma

17.0 Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Programu hii ni kupatikana ufanisi wa huduma za Fedha za Umma. Programu ilitengewa jumla ya TZS 57.86 bilioni. Hadi kufikia Machi 2019, programu ilitumia TZS 28.83 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kutumia TZS 30.0 bilioni kwa kipindi cha miezi tisa. Programu hii inatekelezwa kupitia Programu ndogo tano zifuatazo:

C.4.1.1 Programu ndogo ya Usimamizi wa Hazina

18.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Hazina, hadi kufikia Machi 2019 Programu ilitumia jumla ya TZS 26.28 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kutumia TZS 27.3 bilioni kwa miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa ruzuku ya TZS 26.28 bilioni kwa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mfuko wa Barabara;

ii. Kusimamia ukusanyaji wa Fedha TZS 24.33 bilioni kwa Mfuko wa Miundombinu ambazo ni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya mwaka ya kupokea TZS 39.45 bilioni.

iii. Kusimamia matumizi ya Serikali ya TZS 863.34 bilioni sawa na asilimia 66 ya makadirio ya Bajeti ya mwaka ya TZS 1,315.1 bilioni.

iv. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara katika kada mbali mbali za kihasibu ikiwemo: mafunzo ya CPA na IPSAS;

v. Kutoa mafunzo juu ya usimamizi mzuri wa mfumo wa Malipo ya Mtandao(IFMS) na mafunzo ya Kuimarisha Mfumo wa Matumizi ya Serikali – IFMS;

19.0 Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyotekelezwa kupitia programu ndogo hiyo ni haya yafuatayo:

vi. Kuhudhuria Kongamano la Kimataifa la Wahasibu Wakuu wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAAG);

vii. Kusimamia Deni la Taifa na kufanya usuluhishi wa madeni ya Serikali;

viii. Uimarishaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Matumizi ya Serikali – IFMS;

ix. Kuratibu kazi za Kamati ya Ukomo wa Matumizi Serikalini;

x. Kuhakikisha Wizara na Taasisi zote za Serikali zinatoa risiti za eletroniki;

xi. Kukamilisha utowaji wa huduma ya "Mobile Banking", "Eazy Pesa" na udhibiti kupitia Huduma za Kibenki katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya Kodi kwa Wizara na Taasisi zote zilizobakia.

C.4.1.2 Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali.

20.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii ina lengo la kutayarisha na kusimamia bajeti ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2019 Programu ndogo hii imetumia jumla ya TZS 941.63 milioni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kutumia TZS 975.00 milioni kwa miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuandaa majukwaa ya Bajeti na Uchumi na kuchapisha Mkabala wa bajeti ya mwaka 2019/2020;

ii. Kusimamia utekelezaji ya mwaka 2018/2019;

iii. Kuratibu uandaaji wa Bajeti ya 2019/2020;

iv. Kuandaa warsha ya mafunzo ya bajeti kwa watendaji;

v. Kutoa Mafunzo ya uandaaji wa Bajeti ya Programu kwa Serikali za Mitaa;

vi. Kutoa mafunzo ya MTEF kwa MDAs pamoja na Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti;

vii. Kuwapatia mafunzo wajumbe wa BLW na wajumbe wa Baraza la madiwani juu ya uelewa wa Bajeti ya Serikali;

viii. Kuimarisha mfumo wa taarifa za Mishahara.

C.4.1.3 Programu ndogo ya Uratibu wa Fedha za Nje

21.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii lengo lake ni kuimarisha ufuatiliaji na upatikanaji wa misaada (ruzuku na mikopo) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, Programu ilikadiriwa kutumia TZS 370.41 milioni. Kwa kipindi cha Julai 2018-Machi 2019, Programu imepokea TZS 275.44 milioni sawa na asilimia 93 ya matarajio ya miezi tisa ya kutumia TZS 295.00 bilioni na kutekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia ukusanyaji wa TZS 247.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 53 ya Makadirio ya mwaka;

ii. Kutayarisha mikakati ya kuombewa Fedha za utekelezaji wa Mradi wa Nishati Mbadala kwa Jumuiya ya Ulaya;

iii. Kuratibu mkutano wa majadiliano ya miradi mipya ikiwemo: Mradi wa ujenzi wa matangi ya kuhifadhia mafuta Mangapwani; Mradi wa kuhami misitu ya Zanzibar na wakaazi wa pwani (Safeguarding Zanzibar Forest and Costal habitates);

iv. Kufanya mikutano na BADEA, na kujadili utekelezaji wa miradi inayoendelea kwa kutatua changamoto, kuona uhalisia pamoja na kuangalia maeneo mapya ya mashirikiano;

22.0 Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyotekelezwa kupitia program ndogo hii ni haya yafuatayo:

v. Kushiriki katika mkutano kati ya Shirika la Maendeleo la OPEC(OFID) na Wizara ya Fedha na Mipango ya (Tanzania) kujadili miradi inayofadhiliwa na taasisi hiyo pia kuangalia miradi mipya kwa ajili ya mzunguko mpya wa Fedha 2019-2021;

vi. Kushiriki Mkutano wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kuwasilisha vipaumbele vya miradi mipya itakayofadhiliwa na Benki hiyo;

vii. Kushiriki mikutano ya Nchi wanachama wa Mabadiliko ya Tabia Nchi na fursa ambazo zilipatikana kupitia mikutano hiyo ni utafutaji wa Fedha kupitia Mifuko ya Fedha za Mabadiliko ya Tabia Nchi;

viii. Kushiriki katika mkutano wa mwaka wa Benki ya Dunia nchini Indonesia ambapo ujumbe ulikuwa "kujenga uwezo wa Watu duniani ndio nyenzo kuu itakayomaliza umaskini uliokithiri Duniani";

ix. Kushiriki mkutano wa Baraza kuu la Umoja wa Mataifa (United Nations General Assembly- UNGA) uliolenga kufuatilia majadiliano ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; na

x. Kuratibu maandalizi ya maeneo ya mashirikiano ya muda mrefu na Benki ya Dunia na program mpya ya Maendeleo (Big Z)

C.4.1.4 Programu ndogo ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu

23.0 Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuratibu, kufuatilia, kuwezesha na kusimamia Wakaguzi wa Ndani wa Hesabu wa Serikali kwa madhumuni ya kutoa huduma bora za Ukaguzi wa Ndani Serikalini. Kwa mwaka wa Fedha 2018/19, Programu ilikadiriwa kutumia TZS 1,531.79 milioni. Hadi kufikia Machi 2019, Programu imetumia jumla ya TZS 964.69 milioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha Ripoti za Ukaguzi wa Ndani ya mwaka 2017/2018 katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Miradi ya Maendeleo;

ii. Kuwapatia mafunzo Wakaguzi wa Ndani 120 ya ukaguzi unaozingatia maeneo hatarishi (Risk Based Audit);

iii. Kuwapatia wakaguzi wa Ndani 24 mafunzo ya Kitaaluma (CPA) na Wakaguzi 20 mafunzo ya Mfumo mpya wa Ulipaji wa Serikali (Epicor 10.1);

iv. Kuhudhuria mikutano ya Ukaguzi wa Ndani ya Kitaifa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na ujuzi ambapo kwa Zanzibar wakaguzi 11 walihudhuria.

C.4.1.5 Programu ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi

24.0 Mheshimiwa Spika, lengo la Programu ni kuwa na sera za kodi imara zitakazosaidia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuimarisha uchumi wa nchi. Kwa

mwaka wa Fedha 2018/2019, Programu ilikadiriwa kutumia TZS 783.44 milioni, matumizi halisi kwa kipindi cha miezi tisa yamefikia TZS 368.17 milioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya kutumia TZS 443.00 bilioni kwa miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuzipitia Sheria na Kanuni za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; Wizara Biashara na Viwanda; Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji; Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ili kuchambua na kuainisha vyanzo vya mapato yasiyokuwa ya kodi;

ii. Kuandaa kikao cha Kikosi kazi cha mageuzi ya kodi (Tax Reform Task force); na

iii. Kuchambua na kutathmini ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2018/2019 na kutayarisha makadirio ya mapato ya Serikali kwa mwaka 2019/2020.

25.0 Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyotekelezwa kupitia program ndogo hii ni haya yafuatayo:

iv. Kutoa ushauri wa masuala ya mapato kwa Taasisi na Wizara mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuweka uwiano wa utekelezaji wa Sheria zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato;

v. Kuandaa Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi kwa upande wa Zanzibar;

vi. Kushiriki katika vikao vya Kitaifa, kikanda na Kimataifa juu ya mikakati ya kodi, Fedha na rasilimali za mafuta na gesi;

vii. Kutoa uelewa kwa wadau juu ya tathmini ya udhibiti wa Fedha haramu na ufadhili wa ugaidi nchini;

viii. Kutoa uelewa kwa wadau juu ya matokeo ya utafiti wa hali ya upatikanaji na utumiaji wa huduma za Fedha nchini (FINSCOPE survey Zanzibar), Mpango wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Fedha na Mpango wa Kitaifa wa Elimu ya Fedha.

C.4.2 Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma.

26.0 Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Programu hii ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia mali za Umma na uwekezaji wake. Hadi kufikia Machi 2019 Programu hii imetumia TZS 7.99 bilioni sawa na asilimia 58 ya makadirio kipindi cha miezi tisa ya kutumia TZS 13.94 bilioni. Utekelezaji wa Programu hii umegawika katika Programu ndogo mbili zifuatazo:

C.4.2.1 Programu ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma

27.0 Mheshimiwa Spika, Programu ilikadiriwa kutumia TZS 17.91 bilioni, hadi kufikia Machi 2019 Programu ilitumia TZS 6.91 bilioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya kutumia TZS 12.00 bilioni kwa miezi tisa. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuwapatia mafunzo watendaji juu ya usimamizi wa Mashirika ya Serikali;

ii. Kufuatilia na kuchambua Taarifa za Fedha, Bajeti na Mipango ya biashara ya Mashirika ya Serikali;

iii. Kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Serikali-Gombani Pemba; na

iv. Kukusanya Gawio la TZS 5.80 bilioni kutoka katika Mashirika ya PBZ, ZECO, ZSTC, Bima na Shirika la Bandari.

C.4.2.2 Programu ndogo ya Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali

28.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii ina jukumu la kusimamia Ununuzi na Uondoaji wa mali za Serikali. Katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Programu ilipangiwa kutumia TZS 2.01 bilioni. Hadi kufikia Machi 2019 Programu imetumia TZS 1.08 bilioni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya Julai 2018-Machi 2019. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Kufanya tathmini ya nyumba 860 zitakazoathirika katika mradi wa barabara ya Chake Chake - Wete na kuhakiki nyumba 160 zitakazoathirika katika mradi wa mitaro wa ZUSP katika "system" C;

ii. Kuingiza taarifa za mali 165,427 zilizo chini ya Wizara kumi na nne katika daftari la kielektoniki la Mali za kudumu za Serikali;

iii. Kutoa Mafunzo ya Mfumo wa kielektroni wa Daftari la Usimamizi wa Mali za Serikali (Electronic Fixed Assets Register System) kwa watendaji 25 wa Idara ya Uhakiki Mali.

C.4.3 Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha.

29.0 Mheshimiwa Spika, Programu ina lengo la kuimarisha uendeshaji wa shughuli za sekta ya Fedha. Programu ilikadiriwa kutumia TZS 76.99 bilioni ili kutekeleza shughuli za Wizara na utekelezaji wa Miradi inayosimamiwa na Fungu F01. Kwa kipindi cha miezi tisa programu imetumia TZS 40.42 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Programu hii imeundwa na Programu ndogo tatu zifuatazo:

C.4.3.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara-Unguja

30.0 Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Programu hii ni kusimamia masuala yote ya uendeshaji na utawala wa Wizara na kuimarisha mazingira bora ya kazi. Kwa kipindi cha miezi tisa, jumla ya TZS 5.27 bilioni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya TZS 5.00 bilioni zilitumika ili kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kulipa kwa wakati mishahara ya Wafanyakazi wote wa Wizara;

ii. Kutoa udhamini wa masomo kwa wafanyakazi 18 wa Wizara;

iii. Kuwapeleka mafunzo mafupi ndani na nje ya nchi kwa Wafanyakazi 38 ili kuimarisha ufanisi wa kazi za Wizara;

iv. Kuendesha vikao vya Kamati ya Ukaguzi ya Wizara;

v. Kuendesha mikutano ya Kamati tendaji ya Wizara na mikutano ya Bodi ya Wazabuni ya Wizara; na

vi. Kutekeleza shughuli mbali mbali za Wizara.

C.4.3.2 Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

31.0 Mheshimiwa Spika, lengo la Programu ni kuwa na Mipango na Sera imara ya Sekta ya Fedha itakayosaidia kukuza Uchumi. Programu imetumia TZS 33.27 bilioni sawa na asilimia 81 ya makadirio ya miezi tisa ya kutumia TZS 41.00 bilioni. shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mradi wa ZUSP, Mradi wa Kusaidia Taasisi na Utawala Bora awamu ya tatu (ISPGG III), Mradi wa Kusaidia Taasisi na Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani (ISDRM) ambao utekelezaji wake unaonekana kwenye maelezo ya utekelezaji wa Miradi ya Fungu F01- Wizara ya Fedha;

ii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi na shughuli za Wizara Unguja na Pemba;

iii. Kukamilisha maandalizi ya Sera ya huduma ndogo ndogo za Fedha na kuandaa rasimu ya mswada wa Sheria ya Huduma ndogo ndogo za Fedha (Microfinance);

iv. Kukamilisha matayarisho ya Sheria ya Uwekezaji;

v. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Wizara juu ya masuala Mtambuka ikiwemo: Kujikinga na maradhi ya kuambukiza kama vile Homa ya ini na maradhi ya Ukimwi;

vi. Kuratibu uendeshaji wa vikao 30 vya Bodi ya Rufaa za Kodi; na

vii. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya Sheria, Kanuni za utumishi na kutambua umuhimu wa mikataba ya utoaji wa Huduma.

C.4.3.3 Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Wizara Pemba

32.0 Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Programu ni kupatikana ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba pamoja na kuimarika kwa huduma za sekta ya Fedha. Kutokana na marekebisho ya mshahara program ndogo hii ililazimika kutumia zaidi ambapo hadi Machi 2019 Programu imetumia jumla ya TZS 1.88 bilioni sawa na asilimia 113 ya makadirio ya miezi tisa ya kutumia TZS 1.66 bilioni. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi (12) kwa ngazi ya Diploma, shahada ya kwanza na shahada ya Uzamili.

ii. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi (6) katika vyuo mbalimbali vya ndani ya nchi;

iii. Kuratibu na kusimamia shughuli za usimamizi wa mali za Serikali kwa kuzikagua, kuzithamini na kuziwekea alama za kuzitambua pamoja na kusimamia uondoaji wa mali chakavu kwa Wizara na Taasisi zilizopo Pemba;

iv. Kukagua na kufuatilia shughuli za ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi kwa Wizara na Taasisi pamoja na kusimamia shughuli za kiuhasibu kwa upande wa Pemba; na

v. Kulipa mishahara ya wafanyakazi wa Wizara, Pemba.

33.0 Mheshimiwa Spika, kazi nyengine zilizotekelezwa kupitia programu hii ni hizi zifuatazo:

vi. Kutoa huduma za Hazina ndogo ikiwemo za mtandao wa IFMS kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali pamoja na kuwapatia mafunzo watumiaji wapya wa mtandao;

vii. Kuratibu na kusimamia masuala ya bajeti pamoja na kutoa mafunzo kwa Wahasibu na Maafisa wa Mipango juu ya matumizi ya mtandao wa bajeti;

viii. Kutoa mafunzo ya uandaaji na upitishaji wa bajeti kwa madiwani na wakuu wa Idara na Taasisi;

ix. Kuratibu na kusimamia masuala ya Sera za Fedha na Kodi na ufuatiliaji wa vianzio visivyokuwa vya kodi kwa Ofisi za Wizara sita; na

x. Kusimamia na kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya shughuli za ukaguzi wa ndani pamoja na kufuatilia kazi za wakaguzi wa Wizara na Taasisi.

C.4.4 Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

34.0 Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 134.04 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbamlibali za Mfuko. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai, 2018-Machi, 2019) Programu hii ilipatiwa jumla ya TZS 110.03 bilioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kulipa Riba na Mikopo ya TZS 18.72 bilioni;

ii. Kulipa mafao ya kiinua mgongo cha TZS 25.11 bilioni kwa wastaafu 1,286 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. Kulipa pencheni ya kila mwezi kwa wastani wa wastaafu 13,000 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo jumla ya TZS 19.20 bilioni zimetumika;

iv. Kulipa madeni ya Wazabuni yenye thamani ya TZS 3.80 bilioni; na

v. Kulipa gharama za matumizi mbalimbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jumla ya TZS 43.20 bilioni zimetumika kwa kipindi cha miezi tisa.

35.0 Mheshimiwa Spika, kupitia Tume ya Mipango, Wizara ilitekeleza programu tatu na programu ndogo nane kama ifuatavyo:

C.4.5 Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi

36.0 Mheshimiwa Spika, lengo la Programu ni kuimarisha uratibu wa mipango ya maendeleo pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya kitaifa. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Programu imetumia jumla ya TZS 1.12 bilioni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 1.62 bilioni. Programu hii inatekelezwa kupitia Programu ndogo tatu zifuatazo:

C.4.5.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini

37.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 913.23 milioni. Hadi Machi 2019 Programu hii ilitumia jumla ya TZS 630.44 milioni sawa na asilimia 90 ya makadirio ya miezi tisa. Utekelezaji wa Programu ndogo hii ni kama ifuatavyo:

i. Kujenga uelewa juu ya MKUZA III kwa watendaji zaidi ya 600 wakiwemo: Watendaji Wakuu wa Serikali; Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi; Masheha na Madiwani;

ii. Kuwapatia mafunzo maafisa wanne juu ya upembuzi yakinifu na mafunzo kwa maafisa wawili juu ya usimamizi wa Miradi Tanzania Bara;

iii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango (model Strategic Plan) pamoja na kutoa mafunzo kwa Wakurugenzi na Maafisa mipango wa Wizara

zote na Taasisi za Serikali juu ya uandaaji wa Mpango Mkakati kwa mfumo wa ufuatiliaji wa kupima matokeo (Balance Score Card) ;

iv. Kuvitambua viwanja 1,160 kwa Bint Amran na kufanya malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kupimia ramani (GPS Set);

v. Kuwapatia mafunzo wafanyabiashara 100 juu ya urasimishaji wa biashara katika Wilaya za Wete, Kaskazini B na Halmashauri ya Magharibi A;

vi. Kuratibu uandaaji wa maadhimisho ya wiki ya kupambana na Umasikini kwa kufanya makongamano ya vijana Unguja na Pemba;

vii. Kutafiti Hali ya Umasikini katika shehia 12 za Wilaya ya Mkoani.

38.0 Mheshimiwa Spika, Kufuatia kukaribia kumalizika kwa Dira ya Maendeleo 2020, Wizara imeanza uandaaji wa Dira mpya ya Maendeleo ya Zanzibar hadi mwaka 2050. Kwa kipindi hichi hatua za awali za matayarisho zimeshafanywa zikijumuisha utayarishaji wa Dhana (concept note) na kuundwa kwa Kamati mbili za kufanya tathmini ya Dira 2020 na kuandaa Dira mpya. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kazi ya uandaaji wa Dira mpya ya Maendeleo ya 2050 inakuwa shirikishi na inafanywa kwa ufanisi mkubwa na kuweza kukamilika ndani ya mwaka ujao wa Bajeti 2019/2020.

C.4.5.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu

39.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu kwa mwaka 2018/2019 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 407.3 millioni. Hadi Machi 2019, Programu hii ilitumia jumla ya TZS 234.71 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutathmini mahitaji ya wataalamu Nchini;

ii. Kufuatilia ujazaji wa madaftari ya shehia kwa Shehia 60 kwa Wilaya za Kaskazini B Unguja na Wete Pemba;

iii. Kuwapatia mafunzo washiriki 104 juu ya fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi ya shehia za Wilaya ya Mkoani, Chake chake na Wete Pemba;

iv. Kuchapisha madaftari ya Shehia 1185 na kusambazwa kwa masheha kwa ajili ya kazi ya ujazaji wa kaya za maeneo yao;

v. Kuratibu uendeshaji wa vikao viwili vya wadau wa miradi inayofadhiliwa na UNFPA ili kujadili mafanikio na changamoto za miradi hiyo.

C.4.5.3 Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo

40.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 304.0 milioni.

Hadi Machi 2019, Programu hii ilitumia jumla ya TZS 256.24 milioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya miezi tisa. Shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kufuatilia na kutayarisha ripoti kumi na tano kwa Programu na miradi ya maendeleo kwa vipindi tofauti na kuziwasilisha kwa wadau wakiwemo: Kamati za Baraza la Wawakilishi; Kamati ya Makatibu Wakuu; Tume ya Mipango na Baraza la Mapinduzi;

ii. Kupitia Mipango ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Wizara 14 ili kuhakikisha Programu na miradi ya maendeleo inakuwa na viashiria ambavyo vinapimika na kupata matokeo;

41.0 Mheshimiwa Spika, shughuli nyengine zilizotekelezwa ni hizi zifuatazo:

iii. Kushiriki katika mkutano wa kimataifa, kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu uliofanyika nchini Marekani;

iv. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji 4 wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini juu ya fani ya ufuatiliaji na tathmini huko Tanzania bara;

v. Kujenga uelewa kwa wajumbe wa Kamati 5 za Baraza la Wawakilishi na Wadau 572 kutoka sekta mbali mbali na Serikali za Mitaa Unguja na Pemba juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na kukusanya maoni yao ambayo yamesaidia katika uandaaji wa Ripoti ya Hiari (VNR) juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs);

C.4.6 Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu

42.0 **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu ni kuandaa sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa. Aidha programu imelenga kuharakisha ukuaji na Maendeleo ya kiuchumi, kusimamia uwekezaji binafsi kwa mashirikiano na Serikali (PPP) na kukusanya takwimu sahihi za kiuchumi na kijamii. Hadi kufikia Machi 2019 Programu hii imetumia jumla ya TZS 2.85 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 2.96 bilioni. Programu inatekelezwa kwa Programu ndogo zifuatazo:

C.4.6.1 Programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi

43.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2018/2019 Programu ndogo hii ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 385 milioni. Hadi Machi 2019 Programu hii ilitumia jumla ya TZS 298.23 milioni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kutumia TZS 307.45 milioni kwa kipindi cha miezi tisa. Utekelezaji wa Programu ndogo ni kama ifuatavyo: -

i. Kuandaa ripoti kila mwezi za mwenendo wa uchumi wa Zanzibar;

ii. Kuwapatia mafunzo Wafanyakazi 20 katika modeli za Fedha na Uchumi na wafanyakazi watano katika modeli ya ukadiriaji wa mfumko wa bei;

iii. Kuhudhuria mikutano ya Kamati ya Wataalamu ya uchambuzi wa Deni la Taifa Tanzania Bara;

iv. Kukamilisha tafiti mbili za kisekta na kuwasilisha ripoti ya awali.

C.4.6.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

44.0 **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 80 milioni. Hadi Machi 2019 Programu hii ilitumia jumla ya TZS 44.39 milioni sawa na asilimia 89 ya makadirio ya kutumia TZS 50.0 milioni kwa kipindi cha miezi tisa. Shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wa kitengo cha PPP na Watendaji 30 kutoka Taasisi zinazotekeleza miradi ya PPP ili waweze kuvitambua viashiria hatarishi vinavyoweza kujitokeza katika miradi ya PPP;

ii. Miradi 13 inayopendekezwa kwa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ilitembelewa na kufanyiwa mapitio na uchambuzi kwa kuzingatia vigezo na masharti yake na kupatikana kwa ripoti ya awali; na

iii. Kuanza kwa hatua za matayarisho ya mradi wa nishati mbadala ya jua (Mega Watts 30) utakaotekelezwa na mzalishaji wa umeme wa kujitegemea.

C.4.6.3 Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

45.0 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/2019 Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya TZS 2.94 bilioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi Machi 2019, Programu ndogo

hii imepata jumla ya TZS 2.4 bilioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya miezi tisa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufanya Utafiti wa Hali ya Kiuchumi na Kijamii (Social Economic Survey) wa mwaka 2018 na kuandaa taarifa yake;

ii. Kuendelea na ukusanyaji wa taarifa za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) wa mwaka 2019/2020 pamoja na matayarisho ya Sensa ya kilimo ya mwaka 2018;

iii. Kuratibu na kutoa vibali 270 vya tafiti kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi, kuandaa na kutoa miongozo ya Kitakwimu, Uandishi wa Ripoti za Kitakwimu, Uzalishaji na Uwasilishaji Takwimu, na kupitia Daftari la Taasisi za Kiuchumi na Kijamii.

C.4.7 Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango

46.0 Mheshimiwa Spika, lengo la Programu ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Kwa mwaka 2018/2019, Programu hii ilitengewa jumla ya TZS 1.79 bilioni, ambapo hadi Machi 2019, imetumia jumla ya TZS 1.02 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya miezi tisa. Programu inatekelezwa kupitia Programu ndogo zifuatazo:

C.4.7.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango.

47.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 1,723.9 milioni. Hadi Machi 2019 Programu hii ilitumia jumla ya TZS 966.59 milioni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya miezi tisa. Utekelezaji wa Programu ndogo ni kama ufuatavyo:

i. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ya ndani na nje ya nchi wafanyakazi 23 wa Tume ya Mipango katika fani mbalimbali zinazohusiana na kazi zao;

ii. kuwapatia mafunzo ya ndani (Inhouse training) kwa wafanyakazi 68 Unguja na Pemba juu ya matumizi ya kompyuta na mtandao katika kuleta ufanisi wa kazi;

iii. Kuratibu vikao 11 vikiwemo vitatu vya Tume ya Mipango, viwili vya Kamati ya Wataalamu, vinne vya bodi ya zabuni na viwili vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu;

iv. Kutoa huduma za kiutawala na kiuendeshaji zikiwemo usafiri, ununuzi wa mafuta pamoja na vitendea kazi mbali mbali.

C.4.7.2 Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango-Pemba

48.0 Mheshimiwa Spika, Programu ndogo hii ina lengo la kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya

Ofisi ya uratibu wa Tume ya Mipango Pemba. Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 70 milioni kwa mwaka 2018/2019, ambapo hadi Machi 2019 ilitumia jumla ya TZS 49.93 milioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya miezi tisa.

D. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2018 – MACHI 2019

49.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2018/2019, Wizara imesimamia utekelezaji wa Miradi ifuatayo:

D.1 Mradi wa Kuimarisha Huduma Za Jamii Mijini (ZUSP)

50.0 Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza shughuli za miradi kwa mwaka wa 2018/2019, mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 41.9 bilioni ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi jumla ya TZS 28.5 bilioni zimeshatumika na kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea na kazi ya ujenzi wa jaa la taka la Kibele: Hadi kufikia Machi 2019, tayari kazi hii imeshakabidhiwa Mkandarasi na tayari anaendelea na kazi;

ii. Kuweka taa za barabarani (Street Light II) katika maeneo ya barabara za Uwanja wa ndege-Mnazimmoja; Mwanakwerekwe-Kiembe Samaki na Kinazini- Kariakoo mpaka Kilimani kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba barabara zitakazowekwa taa ni Mkoani bandarini-Kipitacho, Chanjaani – Machomanne, PBZ-Tibirinzi kwa upande wa Chakechake, kwa Wete ni barabara

ya Limbani-maeneo ya Ikulu, Mtemani – Bopwe, Mtemani - Kizimbani. Kazi hii imeshakabidhiwa kwa Mkandarasi kampuni ya Salem Construction Ltd(SALCON) ya Zanzibar kwa upande wa Pemba na kwa Unguja kazi hii itatekelezwa na kampuni STC Construction ltd ya Dar es Salaam. Kwa mujibu wa makubaliano kazi hizi zote zinatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi wa Aprili 2020;

51.0 Mheshimiwa Spika, kazi nyengine zilizotekelezwa kupitia mradi wa ZUSP ni hizi zifuatazo:

iii. Kuendelea na ujenzi wa misingi ya maji ya mvua katika maeneo mbalimbali ya ng'ambo ya mji ambapo hadi Machi 2019 Misingi ya maji ya mvua ya mfumo D ambao unahusisha maeneo ya Kijangwani na Kibandamaiti; mfumo E umeanzia Magomeni, Mpendae, Kwabintiamrani, Meya,Jang'ombe, Migombani hadi Kilimani; Mfumo F huu ni eneo la Mnazimmoja ambao unamwagia maji katika bahari ya Kizingo; Mfumo G ulioanzia Chumbuni, Mtopepo, Karakana na kumwagia maji katika Mtopepo na Mfumo I umeanzia Kwamtipura, Mboriborini, Shaurimoyo, Chumbuni, Mwembemakumbi na kumwaga maji Saateni.

Mheshimiwa Spika, Mifumo hii yote imeshakamilika kwa asilimia 98.82. Msingi uliobakia ni mfumo C ambao bado unaendelea na ujenzi kwa maeneo ya Mwanakwereke, Shaurimoyo, Mikunguni na Saateni. Hadi kufikia Machi mita 5,200 kati ya mita 10,600 za mfumo C zimekamilika na kazi inaendelea; na

iv. Kuimarisha mandhari ya mji (Green Corridor) katika maeneo ya pembezoni mwa barabara ya Malindi-Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil, Mlandege-Maisara na Mkunazini-Kariakoo. Tayari mshauri ameshawasilisha ripoti ya upembuzi yakinifu na kazi ya kutayarisha usarifu wa kina inaendelea.

D.2 Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali

52.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Programu ilipangiwa jumla TZS 15.0 bilioni ambapo hadi kufikia Machi 2019 Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali imeshatumia jumla ya TZS 5.80 bilioni na shughuli zilizofanyika ni:

i. Kukamilisha Ujenzi wa jengo la Ofisi za Serikali Pemba pamoja na uwekaji wa samani na vitendea kazi. Tayari Ofisi hizi zimekamilika na kuanza kutumika; na

ii. Kukamilisha michoro ya jengo la Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango linalotarajiwa kujengwa Mazizini-Unguja.

D.3 Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Mali Asili (ISP-DRMNRG)

53.0 Mheshimiwa Spika, Mradi huu unalenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na mapato kutokana na maliasili zisizorejesheka na unafadhiliwa AfDB. Katika mwaka wa Fedha 2018/2019 mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.27 bilioni ambapo kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 370.8 milioni zimeshatumika sawa na asilimia 8.6 ya makadirio. Mradi umetumia fedha kidogo

kutokana na muda mwingi kutumika katika kukamilisha mchakato wa ununuzi kwa kuzingatia matakwa ya utaratibu wa AfDB. Shughuli zilizotekelezwa ni :

i. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi wa ZURA, ZRB na TRA juu ya uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

ii. Kutafuta washauri kwa kazi kumi tofauti zitakazosaidia kuimarisha mifumo na hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaki wa mapato kwa ZRB;

iii. Kununua vifaa vya ofisi (ICT and office equipment) kwa Mamlaka ya Mapato TRA-Zanzibar na ZURA; na

iv. Kununua vifaa vya Maabara ya ZURA.

D.4 Mradi wa Uimarishaji Utawala Bora Awamu ya tatu (ISPGG III)

54.0 Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la mradi ni ukuzaji na uimarishaji wa masuala ya kifedha na kiuchumi kwa kujenga ufanisi wa usimamizi wa Fedha na kuweka mazingira bora ya biashara nchini. Mradi huu kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, ulitengewa kiasi cha TZS 7.2 bilioni ambapo hadi kufikia robo ya tatu jumla TZS 2.5 bilioni zimeshatumika na miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya kuwajenga uwezo watendaji kwa taasisi zinazonufaika na mradi zikiwemo Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji

wa Mali za Umma, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Fedha za Nje, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na Kitengo cha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP);

ii. Kufanya tathmini ya matumizi ya Fedha za Umma (PEFA);

iii. Kuandaa sera ya sekta binafsi pamoja na mkakati wa utekelezaji;

iv. Kufanya tathmini ya sekta za vipaumbele kwa uwekezaji Zanzibar; na

v. Kuanza uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi wa Maeneo huru ya Kiuchumi ya Micheweni.

D.5 Mradi wa Kuendeleza Bandari ya Mangapwani

55.0 Mheshimiwa Spika, Mradi huu una lengo la kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya barabara, umeme na maji katika eneo la Bandari ya Mafuta na gesi asilia inayokusudiwa kujengwa huko Mangapwani. Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 mradi huu ulipangiwa kutumia kiasi cha TZS 4.2 bilioni. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2019 mradi umeshatumia kiasi cha TZS 74.5 milioni kwa lengo kusafisha eneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara hadi kufikia eneo la bandari. Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo kumepelekea kuchelewa pia uwekaji wa miundombinu ya umeme na maji na hivyo kupelekea matumizi kuwa madogo.

D.6 Mradi wa Kupunguza Umasikini

56.0 Mheshimiwa Spika, Mradi huu umelenga kuwakwamua wananchi na umasikini katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2018/2019, mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 170.00 milioni. Hadi Machi 2019, jumla ya TZS 105.00 milioni sawa na asilimia 62 zimetumika na kutekeleza yafuatayo:

i. Kukamilisha Utafiti wa hali ya umasikini katika shehia 12 za Wilaya ya Mkoani;

ii. Kutoa uelewa kwa wananchi juu ya matokeo ya utafiti wa shehia masikini uliofanyika katika shehia 12 za Wilaya ya Mkoani – Pemba.

57.0 Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatua za awali kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya utafiti wa hali ya umasikini zimeanza kwa kuwapatia mafunzo wananchi wa shehia hizo ili kuanzisha miradi itakayowawezesha kujikwamua na umasikini.

D.7 Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini

58.0 Mheshimiwa Spika, Lengo la mradi huu ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala na idadi ya watu, afya ya uzazi, jinsia na umasikini katika mipango ya maendeleo. Kwa mwaka 2018/2019, mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 197.60 milioni. Hadi Machi 2019, jumla ya TZS 412.0 milioni zimetumika sawa na asilimia 209. Fedha za ziada zimetokana na msaada wa UNFPA kwa Taasisi zinazotekeleza masuala ya Idadi ya Watu ikiwemo Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa

Serikali (OCGS), Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) na Idara ya Watu Wenye Ulemavu.

59.0 Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi hicho, Mradi umetekeleza yafuatayo:

i. Kuingizwa Kaya 2,700 kutoka katika Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" katika mfumo wa kieletroniki wa Daftari la shehia;

ii. Kutoa mafunzo ya ujazaji wa madaftari ya shehia kwa Masheha na wasaidizi wao wa Wilaya ya Magharibi "B" na Kati na Masheha kupewa vitendeakazi kwa ajili ya kuendeleza kazi ya ukusanyaji wa taarifa;

iii. Kutoa matangazo ya uhamasishaji jamii juu ya kutoa taarifa zao kwa watendaji wa shehia yalitayarishwa na kurushwa hewani katika vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na ZBC, TIFFU TV, Tabasam TV na Pemba Cable TV;

iv. Kuchapisha na Kusambaza Madaftari ya shehia 1,185 kwa masheha kwa ajili ya kazi ya ujazaji wa kaya za maeneo yao.

E. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA.

E.1 Bodi ya Mapato-Zanzibar (ZRB)

60.0 Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ni wakala Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya Muungano yanayotokana na vianzio vya

ndani vya kodi. ZRB pia ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusiana na Sera za Kodi. Kwa kipindi cha Julai 2018-Machi 2019, ZRB imetumia TZS 13.5 bilioni na kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kukusanya jumla ya TZS 281.09 bilioni sawa na asilimia 89 ya makadiro ya kukusanya TZS 314.44 bilioni kwa miezi tisa;

ii. Kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Ukusanyaji Kodi katika Hoteli (Hotel Tax Collection Management System - HTCMS) ambao kwa kiasi kikubwa umerahisisha mfumo mzima wa usimamizi wa ukusanyaji kodi katika biashara ya Hoteli. Hadi hivi sasa jumla ya Hoteli 138 zimeshafungiwa mfumo huo katika hatua za awali; na

iii. Kukamilisha michoro ya jengo jipya la Ofisi ya ZRB litakalojengwa Gombani Pemba.

E.2 Mfuko wa Barabara (ZRF)

61.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Mfuko wa Barabara umeendelea na jukumu lake la utunzaji wa Fedha zinazokusanywa kwa ajili ya kufanyia matengenezo ya barabara na kufuatilia matumizi ya Fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na mtandao endelevu wa barabara nchini na kuhakikisha kuwa Fedha hizo zinatumika kwa ufanisi na kwa lengo lililokusudiwa.

62.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Mfuko wa Barabara ulilenga kupokea makusanyo ya jumla ya TZS 15.63 bilioni ambapo TZS 13.54 billioni

zikiwa ni kwa makusanyo yatokanayo na Ada ya Maendeleo ya Barabara TZS 2.01 billioni kutokana na Ushuru wa magari na TZS 84.968 millioni kutokana na ukodishaji wa Jengo. Kati ya Fedha hizo jumla ya TZS 11.96 bilioni zilitengwa kwa kazi za matengenezo ya barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na TZS 2.11 billioni zilitengwa kwa kazi za Matengenezo ya barabara zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ. Aidha, TZS 1.56 billioni zilitengwa kwa kazi za Uendeshaji Mfuko.

63.0 Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya TZS 8.398 billioni zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya kupokea TZS 9.88 bilioni kwa kipindi cha Julai 2018-Machi 2019. Kwa kipindi hicho jumla ya TZS 6.159 bilioni zimetumika na kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Jumla ya TZS 4.417 bilioni zililipwa kwa kazi za Matengenezo ya barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji;

ii. TZS 740.00 millioni zililipwa kwa kazi za Matengenezo ya barabara zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ.

64.0 Mheshimiwa Spika, Barabara zilizohusika na matengenezo hayo ni pamoja na:

i. Mkanyageni – Kangani 5.0 km kiwango cha lami;

ii. Chuo cha Karume- 1.1 km kiwango cha lami;

iii. Kilombero – Mgonjoni 3.5 km iliwekwa kifusi;

iv. Mlilile – Kijibwe 1.2 km uwekaji wa kifusi;

v. Wawi – Mabaoni 3.0 km kiwango cha lami;

vi. Soko Kongwe – Skuli ya Ngomeni 2.1 km kiwango cha lami;

vii. Daraja la Nyumba mbili; na Kalvati ya Kizimbani – Pemba zilifanyiwa ukarabati.

65.0 Mheshimiwa Spika, jumla ya TZS 1.00 bilioni zilitumika kwa kazi za Uendeshaji Mfuko zikiwa ni asilimia 64 ya makadirio ya mwaka.

E.3 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA)

66.0 Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Mamlaka ni kushajiisha Wawekezaji wa Nje na Ndani pamoja na kurahisisha mchakato wa Uwekezaji. Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Mamlaka ilikadiria kukusanya kiasi cha TZS 3.75 bilioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Mamlaka imekusanya jumla ya TZS 1.96 bilioni sawa na asilimia 66 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 2.95 bilioni. Katika makusanyo hayo, TZS 908.82 milioni kutoka vyanzo vyake vya ndani, TZS 646.31milioni ni Ruzuku kutoka Serikalini na TZS 403.98 milioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, hususan Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikiwa ni mikopo yenye masharti nafuu .

67.0 Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilikadiria kutumia jumla ya TZS 3.75 bilioni kwa kazi za kawaida na kazi za

maendeleo. Hadi kufikia Machi 2019, jumla TZS 1.97 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 52.7 ya makadirio ya mwaka zimetumika. Matumizi haya yamejumuisha TZS1.77 bilioni kwa kazi za kawaida ambayo ni sawa na asilimia 60.38 ya makadirio ya mwaka, na TZS 203.82 milioni kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 25 ya makadirio.

68.0 Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hicho cha miezi tisa Mamlaka ilifanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi Fumba;

ii. Kuandaa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi Micheweni (Micheweni Master Plan);

iii. Kuimarisha kituo cha "One Stop Center", maafisa waandamizi wa taasisi zinazotoa huduma kwa wawekezaji wameweza kuhamishiwa ZIPA na kuwa ndio kituo chao cha kazi; na

iv. Kuendelea kusimamia na kuelekeza utekelezaji wa miradi mikubwa na midogo yenye kuleta athari kubwa ya kiuchumi na kijamii nchini.

E.4 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma

69.0 Mheshimiwa spika, lengo la Mamlaka ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ilitengewa ruzuku ya TZS 2.01 bilioni na kukusanya jumla ya TZS 37 milioni kutokana na usajili wa watoa huduma (service

providers). Hadi kufikia Machi 2019, Mamlaka imepokea TZS 1.08 bilioni sawa na asilimia 54 ya makadirio na kukusanya TZS 75.7 milioni sawa na asilimia 202. Ongezeko hilo limetokana na marekebisho mapya ya ada ya usajili ya watoa huduma.

70.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, hadi kufikia mwezi Machi 2019, Mamlaka imetumia jumla ya TZS 1.01 bilioni sawa na asilimia 50 ya makadirio. Kati ya Fedha hizo jumla ya TZS 273.9 milioni zimetumika kwa ajili ya ulipaji wa mishahara sawa na asilimia 31, na TZS 732.6 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo (O/C) sawa na asilimia 65.4.

71.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi 9, Mamlaka imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016 kwa Wizara tatu pamoja na Taasisi tano;

ii. Kufanya ukaguzi wa ununuzi na uondoaji wa mali za Umma katika Wizara ya Biashara na Viwanda; Wizara ya Kilimo, Mali Asili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale;

iii. Kutoa mafunzo kwa Taasisi za Serikali na wahusika wengine juu ya uelewa wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma zikiwemo Kamati za Baraza la Wawakilishi za Fedha, Biashara na Kilimo, Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) na Kamati ya Bajeti.

E.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)

72.0 Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni miongoni mwa Mifuko ya Serikali, ambao umelenga kutoa hifadhi kwa wanachama wake pale wanapofikia umri wa kustaafu au wanapopatwa na majanga ambayo husitisha au kupunguza kipato cha mwanachama. Hivyo katika uendeshaji wa shughuli zake, Mfuko hulipa mafao ya kiinua mgongo na pencheni na kuwekeza ziada ya fedha kwa mujibu wa Sheria nam. 10 ya mwaka 2016 ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

73.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 Mfuko ulikadiriwa kukusanya TZS 116.95 bilioni kutoka michango ya wanachama (TZS 71.45 bilioni) na mapato ya uwekezaji ni TZS 45.49 bilioni. Hadi kufikia Machi 2019 Mfuko umeshakusanya jumla ya TZS 82.65 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Kati ya mapato hayo, michango ya wanachama ni TZS 56.5 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya mwaka na mapato ya uwekezaji ni TZS 26.12 bilioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya mwaka.

74.0 Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi Mfuko ulipanga kutumia Jumla ya TZS 116.95 bilioni ambapo TZS 7.14 bilioni ni gharama za uendeshaji, TZS 30.52 bilioni kwa ajili ya Kulipia Mafao na TZS 79.28 bilioni kwa ajili uwekezaji. Hadi kukamilika kwa robo ya tatu, Mfuko umetumia jumla ya TZS 80.8 bilioni ikiwemo: TZ 5.69 bilioni kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za Mfuko; TZS 22.01 bilioni zimetumika kwa ajili ya ulipaji wa Mafao kwa wanachama; na TZS 53.10 bilioni kwa ajili ya uwekezaji.

E.6 Shirika la Bima (ZIC)

75.0 Mheshimiwa Spika, jukumu la Shirika ni kutoa huduma za Bima kwa wananchi, Kampuni na Mashirika nchini. Katika kipindi cha miezi tisa, Shirika la Bima limekusanya jumla ya TZS 20.2 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio ya kukusanya TZS 21.4 bilioni kwa mwaka.

76.0 Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Shirika limetumia TZS 14.9 bilioni sawa na asimilia 93 ya makadirio ya TZS 16.0 bilioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ulipaji wa madai halali yaliyowasilishwa na yaliyohakikiwa ya TZS 7.9 bilioni;

ii. TZS 1.8 bilioni kwa ulipaji wa ujira kwa mawakala na madalali wa Shirika;

77.0 Mheshimiwa Spika; jumla ya TZS 5.2 bilioni zilitumika kwa matumizi ya kawaida ambapo miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

iii. Uzinduzi wa Ofisi ndogo ya Mauzo katika eneo la Kijitonyama-Dar es Salaam;

iv. Kujenga uelewa kwa wananchi na Taasisi juu ya faida za huduma zinazotolewa na Shirika kwa kupitia vyombo vya Habari; na

v. Kutoa huduma kwa jamii ikiwemo uchimbaji wa visima vya maji kwa jimbo la Tunguu, pamoja na ujenzi wa madrasa kwa maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

E.7 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

78.0 Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Benki ya Watu wa Zanzibar ni kupokea amana za wateja na kuwakopesha wanaohitaji Fedha kwa ajili ya matumizi binafsi au biashara. Aidha, benki inatoa huduma nyengine kama dhamana (guarantee), kufungua Barua za Mikopo (Letter of Credit) na kutuma Fedha ndani na nje ya nchi.

79.0 Mheshimiwa Spika, Rasilimali za benki zimeongezeka kwa asilimia 9 kutoka TZS 602.80 bilioni (2017) hadi TZS 658.40 bilioni (2018). Kuongezeka huku kumesababishwa na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo na uwekezaji katika hati fungani za Serikali. Mikopo imeongezeka kwa TZS 1.84 bilioni sawa na asilimia 0.67 kutoka TZS 272.85 bilioni hadi TZS 274.69 bilioni. Uwekezaji katika hati fungani umeongezeka kwa asilimia 70 kutoka TZS 77.11 bilioni mpaka TZS 130.98 bilioni.

80.0 Mheshimiwa Spika, Ongezeko hilo la uwekezaji limelenga kuongeza ukwasi na uimara wa mtaji (Liquidity & Capital Adequacy). Aidha, amana za wateja zimeongezeka kwa asilimia 5 kutoka TZS 503.93 bilioni (2017) hadi TZS 526.05 bilioni mwaka 2018. Faida kabla ya kodi imeongezeka kwa asilimia 29 kutoka TZS 21.37 bilioni kwa mwaka 2017 na kufikia TZS 27.56 bilioni kwa mwaka 2018.

F. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

F.1 Vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2019/2020

81.0 Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Malengo endelevu ya Dunia (SDGs), Mpango kazi wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/2020. Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kukusanya Mapato ya Ndani ya TZS 976.23 bilioni;

ii. Kusimamia upatikanaji Fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Uwanja wa Ndege "Terminal II" pamoja na matayarisho ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri;

iii. Kuandaa Dira Mpya ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 (Vision 2050);

iv. Kulipia hisa za Kampuni ya Taifa ya Mafuta "Zanzibar Petroleum Development Corporation";

v. Kuimarisha usimamizi wa uchumi utokanao na bahari (Blue Economy);

vi. Kufanya Sensa ya Uzalishaji Viwandani; na

vii. Kufanya Utafiti wa Sekta isiyo Rasmi (Informal Sector).

F.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019-2020

82.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019/2020, Wizara inakadiriwa kukusanya TZS 1,383.05 bilioni ikiwa na ongezeko la asilimia 9 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya TZS 1,273.74 bilioni yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka 2018/2019. Uchambuzi wa Mapato hayo yanayotarajiwa kukusanywa umeambatanishwa katika **Jadweli nam.6.**

83.0 Mheshimiwa Spika; Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara inaombewa matumizi ya jumla ya TZS 389.56 bilioni kwa mafungu ya Wizara ya F01, F02 na F03. Fedha hizo zitatumika kutekeleza shughuli katika Programu kuu saba na Programu ndogo kumi na tisa kama ufuatavyo:

F.2.1 Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma

84.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma imekadiriwa kutumia TZS 120.03 bilioni ambazo zimeelekezwa kutekeleza shughuli za Programu ndogo zifuatazo:

i. Usimamizi wa Hazina inakadiriwa kutumia TZS 40.13 bilioni;

ii. Usimamizi wa Bajeti ya Serikali inakadiriwa kutumia TZS 77.16 bilioni;

iii. Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu unakadiriwa kutumia TZS 1.58 bilioni;

iv. Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi inakadiriwa kutumia TZS 736.58 milioni; na

v. Uratibu wa Rasilimali za Nje inakadiriwa Kutumia TZS 421.47 milioni.

F.2.2 Programu ya Uwekezaji wa Mali za Umma.

85.0 Mheshimiwa Spika; Programu hii imekadiriwa kutumia TZS 20.78 bilioni zitatumika kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Programu ndogo zifuatazo:

i. Usimamizi wa Mitaji ya Umma inakadiriwa kutumia TZS 18.74 bilioni; na

ii. Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali itatumia TZS 2.04 bilioni.

F.2.3 Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango.

86.0 Mheshimiwa Spika, Programu hii imekadiriwa kutumia TZS 79.71 bilioni ambazo zitatumika kutekeleza Programu ndogo zifuatazo;

i. Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha imepangiwa kutumia TZS 70.80 bilioni;

ii. Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Fedha na Mipango imepangiwa kutumia TZS 6.23 bilioni; na

iii. Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Fedha Pemba imepangiwa kutumia TZS 2.68 bilioni.

F.2.4 Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

87.0 Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali inaombewa jumla ya TZS 159.42 bilioni ikijumuisha:

i. TZS 27.6 bilioni zinazotarajiwa kutumika kwa ajili ya ulipaji wa Pencheni;

ii. TZS 30.00 bilioni kwa ajili ya malipo ya Kiinua Mgongo kwa Wastaafu wa Serikali;

iii. TZS 89.18 bilioni kutumika kwa ajili ya matumizi mengine ya Serikali yakiwemo ulipaji wa madeni ya ndani.

F.2.5 Programu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi

88.0 Mheshimiwa Spika, Programu hii imekadiriwa kutumia TZS 4.21 bilioni kutekeleza shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Programu ndogo zifuatazo:

i. Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini imekadiriwa kutumia TZS 1.31 bilioni;

ii. Maendeleo ya Watenda Kazi na Masuala ya Idadi ya Watu imekadiriwa kutumia TZS 703.06 milioni; na

iii. Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo inakadiriwa kutumia TZS 2.21 bilioni.

F.2.6 Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu

89.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Programu inakadiriwa kutumia TZS 4.09 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Programu ndogo nne zifuatazo:

i. Programu ndogo ya Usimamizi wa Uchumi inakadiriwa kutumia TZS 479.31 milioni;

ii. Programu ndogo ya uratibu wa mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi imekadiriwa kutumia TZS 80.0 milioni;

iii. Programu ndogo ya uratibu na kusimamia takwimu-Zanzibar imekadiriwa kutumia TZS 3.43 bilioni; na

iv. Programu ndogo ya Usimamizi wa Uchumi wa Bluu Programu hii ni mpya ikiwa na lengo la kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi zinazotokana na bahari. Kwa kuanzia Programu inakadiriwa kutumia TZS 99.9 milioni ili kutekeleza shughuli za mwaka 2019/2020.

F.2.7 Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango

90.0 **Mheshimiwa Spika,** Programu ya mwisho ni Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango ambayo imekadiriwa kutumia TZS 1.3 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Programu ndogo zifuatazo:

i. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango itatumia TZS 1.10 bilioni; na

ii. Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango-Pemba itatumia TZS 207.26 milioni.

91.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara imepangiwa kutekeleza miradi 13 ambayo inaombewa jumla ya TZS 84.63 bilioni ili kutekeleza shughuli za miradi hiyo. Mahitaji ya Fedha kwa miradi hiyo yameorodheshwa katika **Jadweli nam.8.**

G. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2019/2020 KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA.

G.1 Bodi ya Mapato-Zanzibar (ZRB)

92.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019/2020 Bodi ya Mapato Zanzibar imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 488.5 bilioni, ikiwa ni ongezeko la TZS 82.63 bilioni sawa na asilimia 20.4 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2018/2019 ya kukusanya TZS 405.87 bilioni. Ili kufikia lengo hili mikakati ifuatayo inatarajiwa kutekelezwa:

i. Kuwasajili wafanyabiashara wote na kuhakikisha wanalipa kodi ipasavyo;

ii. Kusimamia utoaji wa stakabadhi za mauzo kwa Wafanyabiasha;

iii. Kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na sekta ya utalii kwa kufanya Ukaguzi katika hoteli;

iv. Kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya ardhi "land lease";

93.0 Mheshimiwa Spika, mambo mengine yatakayotekelezwa na ZRB ni haya yafuatayo:

v. Kuimarisha sehemu ya ukaguzi wa Walipaji kodi kwa kutoa mafunzo ya ukaguzi wa kodi katika sekta ya simu, hoteli na Mafuta;

vi. Kufanya Ukaguzi maalum wa kodi kwa kampuni za simu zinazotoa huduma Zanzibar kwa lengo la kuwalipisha kodi inayostahiki;

vii. Kuanza rasmi matumizi ya utoaji wa risiti za elektroniki kwa kutumia mashine za EFD;

viii. Kutumia rasmi mfumo wa elektroniki wa ukusanyaji katika mahoteli;

ix. Kukamilisha mfumo wa ugawaji wa Zanzibar kimaeneo (Block Management System) ili kurahisisha ukusanyaji kodi; na

x. Kuanza rasmi ukusanyaji wa kodi ya majengo.

94.0 Mheshimiwa Spika, Ili kutekeleza majukumu yake, ZRB inaombewa ruzuku jumla ya TZS 27.12 bilioni.

G.2 Mfuko wa Barabara (ZRF)

95.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha wa 2019/20 Mfuko unaombewa ruzuku jumla ya TZS 15.139 bilioni. Ruzuku hiyo itatumika kama ifuatavyo:

i. Matengenezo ya barabara kuu yanakadiriwa kutumia TZS 11.521 billioni. Matengenezo ya Barabara kuu yatahusisha barabara zifuatazo: Fuoni Mambosasa - Mwera (3.4 km); Kinduni - Kichungwani (4km); Kiembesamaki -Mnazimmoja (2.5 km) na Finya - Kicha (4.4 km);

ii. Matengenezo ya dharura ya barabara yanatarajiwa kutumia TZS 2.033 billioni na;

iii. TZS 1.585 billioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kuendesha kazi za kawaida za Mfuko.

G.3 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA)

96.0 Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2019/2020 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji inatarajia kukusanya TZS 3.8 bilioni ambapo kiasi cha TZS 2.60 bilioni zitatoka katika vyanzo vyake vya ndani na TZS 562.60 milioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na inaombewa TZS 650.00 milioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

97.0 Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa Sheria Mpya ya Uwekezaji inatekelezwa ipasavyo na kutimiza malengo ya Dira ya Maendeleo 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar na Ilani ya uchaguzi ya CCM 2015/2020. Katika bajeti ya mwaka 2019/2020, Mamlaka imeelekeza nguvu zake katika kutimiza vipaumbele vya MKUZA III.

i. Kukamilisha utafiti wa Sekta za kipaumbele kwa uwekezaji nchini;

ii. Kuendeleza miundombinu ya barabara, maji, umeme na huduma nyengine katika maeneo huru ya kiuchumi;

iii. Kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkuu wa maeneo huru ya kiuchumi ya Micheweni; na

iv. Kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta zitakazobainishwa na matokeo ya utafiti.

G.4 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma

98.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2019-2020, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma imekadiriwa kukusanya TZS 300.00 milioni kutoka katika vianzio vyake. Pia, Mamlaka inaombewa ruzuku ya TZS 1.91 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza shuguli zifuatazo:

i. Kuendelea kufanya ukaguzi na uchunguzi wa ununuzi na uondoaji wa mali za Umma kwa Wizara nane;

ii. Kuandaa na kutoa Miongozo sita ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma;

99.0 Mheshimiwa Spika, mambo mengine yatakayotekelezwa ni haya yafuatayo:

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 12 wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi;

iv. Kuendelea Kutoa mafunzo juu ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma pamoja na Kanuni kwa Watendaji wakuu wa Wizara (Accounting Officers) pamoja na wajumbe wa Bodi za Zabuni za Serikali;

v. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi zinazojishughulisha na ununuzi na uondoaji wa mali za Umma Tanzania Bara; na

vi. Kuendelea kushirikiana na wahusika mbalimbali katika kuimarisha mfumo wa Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwa njia ya eletroniki.

G.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)

100.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019 /2020 Mfuko unategemea kukusanya mapato ya jumla TZS 138.50 bilioni kutokana na vyanzo vikuu wiwili, ambapo TZS 85.50 bilioni kutokana na makusanyo ya michango ya wanachama na TZS 53.00 bilioni kutokana na mapato ya uwekezaji.

101.0 Mheshimiwa Spika, Mfuko unategemea kutumia Jumla ya TZS 138.5 bilioni kwa matumizi yake ya mwaka 2019/2020 ambapo TZS 8.20 bilioni zinategemewa kutumika kwa matumizi ya uendeshaji, TZS 37.26 bilioni kulipia mafao ya wanachama na TZS 93.10 bilioni kwa ajili ya uwekezaji. Shughuli za uwekezaji zitakazotekelezwa ni :

i. Kuendelea na ujenzi wa Michenzani Mall kwa kuwekwa "slab"na kusimamisha ghorofa ya tatu hadi ya saba;

ii. Kuendelea na ujenzi wa Mwembekisonge;

iii. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makaazi ya Mbweni kwa kukamilisha majengo sita ya awamu ya pili na kufanya idadi ya majengo yaliyokamilika kuwa kumi na tano;

iv. Kuendeleza ujenzi wa Hoteli ya Mkoani;

v. Kuanza ujenzi wa Ofisi ya ZSSF Pemba; na

vi. Kuwekeza amana ya TZS 31.00 bilioni kwa muda maalum katika soko la Fedha la ndani.

G.6 Shirika la Bima (ZIC)

102.0 Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima kwa mwaka 2019/2020 linatarajia kukusanya jumla ya TZS 28.8 bilioni kutoka katika vianzio vyake vya mapato Shirika limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kutoa taaluma kwa wananchi na taasisi mbalimbali juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao;

ii. Kuzidisha mashirikiano kwa mawakala na madalali na kuwapatia vivutio zaidi;

iii. Kufuatilia matatizo ya wateja baada ya kuwapa huduma;

iv. Kuongeza idadi ya wateja wa biashara zisizokuwa za magari katika mtandao wa Shirika.

103.0 Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya TZS 20.6 bilioni ikijumuisha matumizi yafuatayo:

i. Matumizi kwa kazi za kawaida ya kuendesha shughuli za Shirika ni TZS 7.7 bilioni;

ii. Matumizi kwa kazi za maendeleo ni TZS 3.9 bilioni. Fedha hizi zimepangiwa kukidhi mahitaji ya ununuzi wa vitendea kazi Makao Makuu na ofisi zote za kanda, ununuzi wa mtandao mpya wa Shirika, ujenzi wa jengo jipya Pemba, kufanya tathmini ya Mfuko wa Shirika (General Insurance Fund), na ununuzi wa gari mpya kwa matumizi ya Shirika; na

iii. Ulipaji fidia kwa madai halali ya wateja ambayo yanakadiriwa kufikia TZS 9.0 bilioni.

G.7 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

104.0 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019, PBZ inatarajia kuimarisha utoaji wa huduma kwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuimarisha mfumo mpya wa kibenki ili kubaini dosari na kuzirekebisha;

ii. Kuanza kutoa huduma za kadi za kimataifa (Visa na Master Card);

iii. Kutoa huduma za kibenki kwa kutumia mawakala;

iv. Kuweka mfumo wa kupima utendaji wa wafanyakazi;

v. Kuanza na kukamilisha ujenzi wa Tawi pacha la Malindi;

vi. Kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Benki ya Watu wa Zanzibar hapo Mazizini;

vii. Kufunga mashine za ATM kumi na nne katika maeneo ya Gombani, Mtambile, Wete kwa upande wa Pemba; Amani, Kwamchina na Mwera kwa upande wa Unguja na Dar es Salaam mashine zitafungwa katika mitaa ya Tandika na Kigamboni.

105.0 Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya mwaka 2019 PBZ inakadiria kutumia TZS 30.65 bilioni kwa matumizi ya kawaida na TZS 21.00 bilioni kwa kazi za maendeleo.

106.0 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka imepangiwa kukusanya TZS 350.19 bilioni kwa hapa Zanzibar na kuingizwa kwenye Mfumo wa Serikali.

H. SHUKRANI

107.0 Mheshimiwa Spika, kabla ya kukamilisha hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, naomba kuzishukuru taasisi na Washirika wa Maendeleo waliojitolea kuisaidia Wizara na Serikali kwa ujumla kuweza kutekeleza majukumu yaliolenga kuleta Maendeleo kwa nchi yetu. Aidha nachukua fursa hii kuzishukuru taasisi na Asasi za kiraia pamoja na sekta binafsi kwa mashirikiano yao makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

108.0 Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Nd. Khamis Mussa Omar, Katibu Mtendaji-Tume ya Mipango Nd. Juma Hassan Reli, Naibu Katibu Mkuu- Nd. Iddi Haji Makame, Mhasibu Mkuu wa Serikali Nd. Mwanahija Almas Ali pamoja na Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao wanazozichukua ili kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Wananipa mashirikiano ya kutosha tangu niingie kwenye Wizara hii Machi, 2019.

109.0 Mheshimiwa Spika, ninawashukuru wananchi wote wa visiwa vya Zanzibar kwa kudumisha Amani ya Nchi yetu ambayo inatuwezesha kutekeleza shughuli zetu za Maendeleo kwa ufanisi.

110.0 Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa shukrani maalum. Katika uendeshaji wa Serikali Ofisi zinaendeshwa kwa kupokezana majukumu. Kwa miaka mitatu iliyopita, Wizara hii iliongozwa kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa. Dkt. Khalid Mohamed Salum, Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Donge. Namshukuru sana kwa kazi kubwa aliyoifanya katika muda wote aliotumikia nafasi hii na kujenga msingi imara ambao umenirahisishia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Khalid kwa kazi nzuri na namshukuru sana.

I. HITIMISHO

111.0 Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo niliyoyatoa, sasa naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kuridhia maombi ya Wizara ya kukusanya jumla ya wa Mapato ya TZS 1,383.05 bilioni kwa mwaka 2019/2020. Ili Wizara

iweze kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka huu, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya TZS 389.56 bilioni.

112.0 Mheshimiwa Spika, Maelezo na shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka huu yanapatikana katika kitabu cha tatu (Volume 3) cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa Fedha 2019/2020-2021/2022 katika ukurasa wa F-1 hadi F03-13 .

113.0 Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)
WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO;
ZANZIBAR.

VIAMBATANISHO VYA UTEKELEZAJI JULAI 2018-MACHI 2019

Jadweli nam.1

Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango

IDARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO		
FUNGU	**IDARA ZA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**	**TAASISI ZINAZOJITEGEMEA**
F01: WIZARA YA FEDHA	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)
	Idara ya Bajeti	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)
	Idara ya Fedha za Nje	Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA)
	Idara ya Uhakikimali	Mfuko wa Barabara (ZRF)
	Idara ya Mitaji ya Umma	Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)
	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	Bodi ya Rufani za kodi (Tax Apeal Board)
	Idara ya Hesabu za Ndani	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF
	Idara ya Utawala na uwendeshaji	Mahakama ya Rufani za Kodi
	Idara ya Fedha na Kodi	Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.
	Ofisi Kuu Pemba	
F02: MFUKO MKUU WA SERIKALI	Mfuko Mkuu wa Serikali	
	Idara ya uratibu wa mipango ya kitaifa, maendeleo ya kisekta na kupunguza umaskini	Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
	Idara ya maendeleo ya Watendakazi	
	Idara ya Ukuzaji Uchumi	
	Idara ya Usimamizi wa Uchumi wa Bluu	
	Idara ya Ufatiliaji na Tathmini	
F03: TUME YA MIPNGO		
TAASISI ZA MUUNGANO		
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)-Tawi la Zanzibar		
Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA)-Tawi la Zanzibar		
Benki Kuu ya Tanzania (BOT)-Tawi la Zanzibar		
Tume ya pamoja ya Fedha-Tawi la Zanzibar		

Jadweli nam.2

Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2018-Machi 2019

Maelezo	Makadirio 2018/2019	Ukusanyaji Halis	% PER B
Mapato			
ZRB	405.4	281.09	69%
TRA	301.1	216.28	72%
PAYE	21	14	67%
Mapato ya Mawizara	76	51.028	67%
Gawio la BOT	4	15.75	394%
Mikopo	40	32	80%
GBS/MDRI		6.38	
Jumla ndogo	**847.5**	**616.528**	**73%**
Fedha kutoka ODA	464.12	247.97	53%
	1311.62	**864.498**	**66%**
Matumizi ya Serikali			
Mishahara	232.54	169.72	73%
Mfuko Mkuu wa Serikali	132.75	110.03	83%
Ruzuku ya Mshahara	104.58	78.03	75%
Ruzuku ya OC	84.92	61.56	72%
Matumizi Mengineyo	147.37	116.41	79%
Jumla ndogo	**702.16**	**535.75**	**76%**
Mchango wa Serikali katika Shughuli za Maendeleo	148.75	83.01	56%
Mchango wa Shughuli za Maendeleo kutoka ODA	464.12	244.58	53%
Jumla ya matumizi ya Maendeleo	**612.87**	**327.59**	**53%**
Jumla kuu ya Matumizi	**1315.03**	**863.34**	**66%**

Chanzo: Ofisi za Mhasibu Mkuu wa Serikali

I.1 *Jadweli nam.3. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya ndani kuelekea 2020*



Jadweli nam.4

Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango Julai 2018-Machi 2019.

Mapato yaliyopangwa kukusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19					
Tarakimu ni bilioni					
Vianzio	Makadirio 2018/19	Makadirio Julai 2018-Machi 2019	Halisi Julai - Machi 2019	Asilimia kwa Bajeti	Asilimia kwa miezi 9
Mapato ya Kodi					
ZRB	405.4	314.44	281.09	69%	89%
TRA	301.1	221.05	216.27	72%	98%
PAYE	21.00	15.75	14.00	67%	89%
Mapato ya kodi	**727.50**	**551.24**	**511.36**	**70%**	93%
Mikopo ya ndani	40.00	30.00	32.00	80%	107%
Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo	464.20	348.08	247.97	53%	71%
Jumla ndogo	**1,231.70**	**929.32**	**791.33**	**64%**	85%
Mapato yasiyokuwa ya kodi					
Gawio kutoka katika Mashirika na Benki Kuu	9.00	9.00	15.75	175%	175%
Mapato ya Uhamiaji	27.56	25.62	21.98	80%	86%
Uuzaji wa vifaa chakavu	0.29	0.18	0.22	76%	122%
Mapato yatakayokusanywa kutokana na utakasishaji fedh	0.756	0	0	0%	
Mchango wa fedha kutoka ZURA	3.00	1.96	2.00	67%	102%
Kodi za nyumba za Serikali	0.85	0.52	0.33	39%	63%
Kodi ya Bohari	0.58	0.46	0.31	53%	67%
Jumla ndogo	**42**	**38**	**41**	**97%**	108%
Jumla Kuu	**1,273.74**	**967.06**	**831.92**	**65%**	86%
Chanzo: Sehemu ya hesabu - WF					

Jadweli nam.5

Matumizi ya Wizara kwa Programu-Julai 2018-Machi 2019

S/N	Program kuu	Program ndogo	Makadirio kwa mwaka 2018/2019	Makadirio kwa Juali-Machi	Fedha iliyopatikana Julai 2018-Machi 2019	Asilimia kwa mwaka kwa mwaka	Asilimia kwa miezi 9
			Tarakimu ni milioni				
1	Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	Usimamizi wa hazina	39,065.75	27,300.00	26,285.03	67%	96%
		Usimamizi wa Bajeti ya Serikali	1,107.24	975.00	941.63	85%	97%
			15,000.00				
		Uratibu wa Rasilimali za nje	370.41	295.00	275.44	74%	93%
		Usimamizi wa hesabu za ndani	1,531.79	985.00	964.69	63%	98%
		Usimamizi wa sekta ya Fedha na Kodi	783.44	443.00	368.17	47%	83%
		Jumla ndogo	**57,858.63**	**29,998.00**	**28,834.96**	**50%**	**96%**
2	Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma	Usimamizi wa Mitaji ya Umma	17,909.54	12,000.00	6,911.51	39%	58%
		Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa mali za Serikali	2,010.00	1,940.00	1,076.57	54%	55%
		Jumla ndogo	**19,919.54**	**13,940.00**	**7,988.08**	**40%**	**57%**
3	Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango	Utawala na Uendeshaji wa Wizara	5,328.69	5,000.00	5,272.51	99%	105%
		Kuandaa Mipango, Sera na kufanya tafiti za Sekta ya Fedha	69,911.88	41,000.00	33,265.18	48%	81%
		Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba	1,745	1,659.00	1,881.44	108%	113%
		Jumla ndogo	**76,985.83**	**47,659.00**	**40,419.13**	**53%**	**85%**
		Jumla F01	**154,764.00**	**91,597.00**	**77,242.17**	**50%**	**84%**
4	Usimamizi wa mfuko Mkuu wa Serikali	**Jumla F02**	**134,035.30**	**105,000.00**	**110,030.10**	**82%**	**105%**
5	Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi	Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini	913.23	702.00	630.44	69%	90%
		Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya watu	407.27	314.00	234.71	58%	75%
		Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo	304.00	266.00	256.24	84%	96%
		Jumla ndogo	**1,624.50**	**1,282.00**	**1,121.39**	**69%**	**87%**
6	Usimamizi wa uchumi Mkuu	Usimamizi wa Uchumi Mkuu	3,323.00	2,906.00	2,807.84	84%	97%
		Mashirika baina ya Sekta za umma na Binafsi	80.00	50.00	44.39	55%	89%
		Jumla ndogo	**3,403.00**	**2,956.00**	**2,852.23**	**84%**	**96%**
	Utawala na uendeshaji wa Tume ya Mipango	**Jumla ndogo**	**1,793.90**	**1,200.00**	**1,016.52**	**57%**	**85%**
		Jumla F03	**6,821.40**	**5,438.00**	**4,990.14**	**73%**	**92%**
		Jumla Kuu	**295,620.70**	**202,035.00**	**192,262.41**	**65%**	**95%**

J. VIAMBATANISHO VINAVYOHUSU MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019-2020

Jadweli nam.**6**

Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019-2020

Mapato yaliyopangwa kukusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/2020			
			Tarakimu ni bilioni
Vianzio	**Makadirio 2018/19**	**Makadirio 2019/20**	**Ongezeko**
Mapato ya Kodi			
ZRB	405.4	488.5	20%
TRA	301.1	350.19	16%
PAYE	21.00	21.00	0%
Mikopo ya ndani	40.00	40.00	0%
Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo	464.20	402.91	-13%
Jumla ndogo	**1,231.70**	**1,302.60**	6%
Mapato yasiyokuwa ya kodi			
Gawio kutoka katika Mashirika na Benki Kuu	9.00	17.50	94%
Mapato ya Uhamiaji	27.56	55.60	102%
Uuzaji wa vifaa chakavu	0.29	0.49	68%
Mapato yatakayokusanywa kutokana na utakasishaji fedh	0.756	0.10	-87%
Mchango wa fedha kutoka ZURA	3.00	4.80	60%
Kodi za majengo ya Serikali	0.85	0.79	-7%
Kodi ya Bohari	0.58	0.74	28%
Uuzaji wa nyaraka za Zabuni		0.05	
Usajili wa Wazabuni		0.30	
Uuzaji wa mabuku ya Stakabadhi		0.07	
Jumla ndogo	**42**	**80**	91%
Jumla Kuu	**1,273.74**	**1,383.05**	9%
Chanzo: Ofisi za Idara ya Bajeti-WFM			

Jadweli nam.7-Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango 2019-2020 kwa Programu

S/N	Program kuu	Program ndogo	Makadirio kwa mwaka 2018/2019	Makadirio kwa mwaka 2019/2020	Ongezeko la Bajeti
			Tarakimu ni TZS milioni		
1	Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	Usimamizi wa hazina	39,065.75	40,128.03	3%
		Usimamizi wa Bajeti ya Serikali	16,088.15	77,164.42	380%
		Uratibu wa Rasilimali za nje	370.41	421.47	14%
		Usimamizi wa hesabu za ndani	1,531.79	1580.8	3%
		Usimamizi wa sekta ya Fedha na Kodi	802.02	736.58	-8%
		Jumla ndogo	**57,858.12**	**120,031.30**	107%
2	Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma	Usimamizi wa Mitaji ya Umma	17,909.54	18,739.83	5%
		Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa mali za Serikali	2,010.00	2,039.08	1%
		Jumla ndogo	**19,919.54**	**20,778.91**	4%
3	Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango	Utawala na Uendeshaji wa Wizara	5,328.69	6,233.90	17%
		Kuandaa Mipango, Sera na kufanya tafiti za Sekta ya Fedha	69,911.88	70,799.55	1%
		Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba	1,746.76	2,678.73	53%
		Jumla ndogo	**76,987.33**	**79,712.18**	4%
		Jumla F01	**154,764.99**	**220,522.39**	42%
4	Usimamizi wa mfuko Mkuu wa Serikali	**Jumla F02**	**132,750.00**	**159,417.70**	20%
5	Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi	Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini	913.23	1,306.03	43%
		Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya watu	407.27	703.06	73%
		Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo	304.00	2,205.69	626%
		Jumla ndogo	**1,624.50**	**4,214.78**	159%
6	Usimamizi wa uchumi Mkuu	Usimamizi wa Uchumi Mkuu	385.00	479.31	24%
		Mashirika baina ya Sekta za umma na Binafsi	80.00	80.00	0%
		Usimamizi wa Uchumi wa Bluu		99.90	
		Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Takwimu Zanzibar	2,938.00	3,434.70	17%
		Jumla ndogo	**465.00**	**4,093.91**	780%
	Utawala na uendeshaji wa Tume ya Mipango	Utawala na uendeshaji wa Tume ya Mipango-Unguja	**1,753.90**	**1,102.41**	-37%
		Uratibu na na uendeshaji wa Tume ya Mipango-Pemba	**40.00**	**207.25**	418%
		Jumla ndogo	**1,793.90**	**1,309.66**	-27%
		Jumla F03	**3,883.40**	**9,411.10**	142%
		Jumla Kuu	**291,398.39**	**389,351.19**	34%

Jadweli nam.8-Makadirio ya Matumizi ya Fedha katika Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango

MIRADI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO 2019/20 TZS "000"									
FUNGU	JINA LA PROGRAMU/MRADI	MAKISIO KWA MWAKA 2018/2019 SMZ	MAKISIO KWA MWAKA 2019/20 SMZ			MICHANGO YA WAHISANI			JUMLA YA BAJETI
			MAKISIO YA KAWAIDA 2019/20	DHIMA 2019/20	JUMLA YA MAKISIO YA SMZ 2019/20	MUHISANI	RUZUKU	MIKOPO	
F01	WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO								
	Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar	15,000,000		10,002,300	10,002,300				10,002,300
	Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)					WORLD BANK		57,407,042	57,407,042
	Programu ya Upatikanaji Rasilimali Fedha	1,000,000	300,000		300,000				300,000
	Programu ya Kuimarisha Maendeleo Endelevu (UNDAP II)	50,000	50,000		50,000	UNDP	1,585,990		1,635,990
	Miradi								
	i) Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Tatu	150,000	100,000		100,000	AfDB		4,013,767	4,113,767
	ii) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili	100,000	50,000		50,000	AfDB		2,523,642	2,573,642
	iii) PFMRP					NORWAY	1,598,719		1,598,719
	iv) Mradi wa Kuendeleza Bandari ya Mangapwani	4,200,000	4,000,000		4,000,000				4,000,000
	JUMLA YA FUNGU	20,500,000	4,500,000	10,002,300	14,502,300		3,184,709	63,944,451	81,631,460
F03	TUME YA MIPANGO								
	Programu ya UNDAP								
	i) Kupunguza Umasikini na Ufuatiliaji wa SDGs	180,000	230,000		230,000				230,000
	ii) Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Malengo na Maendeleo Endelevu (SDGs) na MKUZA III		20,000		20,000	UNDP	1,689,079		1,709,079
	Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)	200,000	500,000		500,000	URT	168,883		668,883
	Miradi								
	i) Kuendeleza Tafiti na Ubunifu	200,000	0		-				0
	ii) Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu katika Afya ya Uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini	29,000	0		-	UNFPA	400,400		400,400
	JUMLA YA FUNGU	609,000	750,000	0	750,000		2,258,362	0	3,008,362

Chanzo: Tume ya Mipango-Zanzibar.

VIFUPISHO

ACGen	:	Accountant General
AfDB	:	African Development Bank
BADEA	:	Banque Arabe pour le Development Economique en Afrique
BLW	:	Baraza la Wawakilishi
CPA	:	Certified Public Accountants
CRJE	:	China Railway Jianchang Engineering
DEF	:	Department of External Finance
DFID	:	Department for International Development
ESAAG:		Eastern and Southern Africa Association of Accountant General
EU	:	European Union
FINSCOPE	:	Financial Scope
GPS	:	Global Positioning System
HBS	:	Household Budget Survey
ICT	:	Information and Communication Technology
IFMS	:	Integrated Financial Management System
IMF	:	International Monetary Fund
IPSAS	:	International Public Sector Accounting
ISDRM	:	Institutional Support for Domestic Resources Mobilization
ISPGG III	:	Institutional Support Project for Good Governance
MDAs	:	Ministries Department and Agencies
MKUZA III	:	Mkakati wa Kupunguza Umasikini Zanzibar
MTEF	:	Medium Term Expenditure Framework
MTIM	:	Ministry of Trade, Industry and Marketing
OCAG	:	Office of Controller and Auditor General
OCGS	:	Office of Chief Government Statistician
OFID	:	OPEC Fund for International Development
PAC	:	Public Account Committee

PBZ	:	People's Bank of Zanzibar
PEFA	:	Public Expenditure Financial Assessment
PPP	:	Public Private Partnership
		Resources Mobilized
SDGs	:	Sustainable Development Goals
		Standards
UNICEF	:	United Nation International Children Emergency Fund
VNR	:	Voluntary National Report
ZAECA	:	Zanzibar Anti-corruption and Economic Crime Authority
ZBC	:	Zanzibar Broadcasting Corporation
ZCSRA	:	Zanzibar Civil Status Registration Agency
ZECO	:	Zanzibar Electricity CorpOration
ZIC	:	Zanzibar Insurance Corporation
ZIPA	:	Zanzibar Investment Promotion Authority
ZPPDA	:	Zanzibar Public Procurement and Disposal
ZRB	:	Zanzibar Revenue Board
ZRF	:	Zanzibar Road Fund
ZSSF	:	Zanzibar Social Security Fund
ZSTC	:	Zanzibar State Trading Cooperation
ZURA	:	Zanzibar Utility Regulatory Authority
ZUSP	:	Zanzibar Urban Services Project